JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

Unapojibu tafadhali taja:

Wananchi wote,
Tanzania bara na visiwani.

KUMB. NA. HB/A: 20/1.VOL.II/589

29.02.2024

**MARUDIO YA TANGAZO LA YA NAFASI ZA KAZI ZA DEREVA, MUUGUZI NA RADIOLOJIA**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Bunda anapenda kuwatangazia Watanzania wote Bara na Visiwani wenye sifa kuomba nafasi za kazi zilizoorodheshwa hapo chini.

1. **DEREVA DARAJA II - NAFASI MOJA (1)**

**(a). SIFA ZA WAOMBAJI**

- Awe amehitimu elimu ya kidato cha nne (IV) au cha sita (VI)
- Awe na leseni ya udereva daraja E au $C_1$ ya uendeshaji magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja (01) bila kusababisha ajali.
- Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji magari (Basic Driving Course) yanayotolewa na chuo cha mafunzo ya ufundi stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambulika na serikali.
- Waombaji wenye cheti cha majaribio ya ufundi Daraja la II watafikiriwa kwanza.

**(b). KAZI NA MAJUKUMU:**

- Kuendesha gari la wagonjwa (Ambulance)
- Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kibaini hali ya usalama wa gari
- Kusafirisha wagonjwa wa rufaa na wasindikizaji kwenda katika vituo vya tiba vitakavyoainishwa kulingana na rufaa husika.
- Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari
- Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (Log book).
- Kufanya usafi wa gari
- Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na Mkuu wake wa kazi.

NB: Ajira itakuwa ya mkataba wa mwaka mmoja (01) inayoweza kuhuishwa (renewable). Kwa kipindi chote cha mkataba Mganga Mfawidhi wa kituo atagharamia ajira hiyo.

**(c). NGAZI YA MSHAHARA -**

- Mshahara utakuwa ni shilingi Tzs. 350,000.00 kwa mwezi.



CamScanner

2. MUUGUZI DARAJA LA II - NAFASI MOJA (1)

(a) SIFA ZA WAOMBAJI

- Awe na cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika chuo kinachotambuliwa na Serikali
- Awe ameandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

NB: Ajira itakuwa ya mkataba wa miezi sita (06) kwa kipindi chote mradi wa UVIKO 19 utagharamia ajira yake.

(b). KAZI NA MAJUKUMU:

i. Kufanya kazi za kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya.
ii. Kusimamia na kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi.
iii. Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi.
iv. Kutoa huduma kwa wagonjwa majumbani.
v. Kutoa ushauri nasaha.
vi. Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango.
vii. Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto.
viii. Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya.
ix. Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi.
x. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na ujuzi wake na uzoefu kazini.

(c). NGAZI YA MSHAHARA

- Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali yaani TGHS $A_1$ (Tzs. 492,000.00) kwa mwezi.

3. MTEKNOLOJIA (RADIOLOJIA) DARAJA LA II – NAFASI MOJA (01)

(a) SIFA ZA WAOMBAJI:

- Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika radiolojia kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.
- Awe amesajiliwa na Baraza linalohusika.

(b). KAZI NA MAJUKUMU:

i. Kuwapima wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi
ii. Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi
iii. Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality)
iv. Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa
v. Kusimamia watumishi walio chini yake
vi. Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.
vii. Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization)
viii. Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.



CamScanner

ix. Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**(c). NGAZI YA MSHAHARA**

- Kwa kuzingatia ngazi ya Mishahara ya Serikali yaani TGHS $B_1$ (Tzs. 740,000.00) kwa mwezi.

NB: Ajira zitakuwa za mkataba wa mwaka mmoja (01) inayoweza kuhuishwa (renewable) kwa kipindi chote ambacho Waganga Wafawidhi wa Vituo watagharamia ajira hizo.

**MASHARTI KWA UJUMLA**

- Waombaji wote wawe ni Raia wa Tanzania na wenye umri wa kuanzia miaka 18 na usiozidi miaka 45.
- Waombaji wote waambatishe nakala ya cheti cha kuzaliwa na kitambulisho cha Uraia (NIDA) au namba ya NIDA kwa ambao hawajapata Kitambulisho.
- Waombaji wote waambatishe maelezo binafsi (Detail CV) yenye anuani na namba za simu zinazopatikana pamoja na majina ya wadhamini watatu (Referees) wa kuaminika.
- Maombi yote yaambatane na vyeti vya Elimu na Taaluma yaani nakala ya vyeti vya Kidato cha Nne au Sita pamoja na vyeti vya taaluma (Professional Certificate from respective Board, computer certificate) na picha mbili za rangi za hivi karibuni.
- Testmonial, provisional results, Statement of results, hati ya matokeo ya Kidato cha Nne (Form IV) na Kidato cha Sita (Form VI) **havitakubalika kabisa.**
- Waombaji waliosoma nje ya Tanzania wahakikishe vyeti vyao vimehakikiwa na kuidhinishwa na Mamlaka husika (NECTA na NACTE) na taarifa ya ulinganifu iambatishwe kwenye maombi.
- Waombaji wa nafasi za ajira waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana kibali kutoka kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.
- Barua ya maombi iandikwe kwa mkono na kwa lugha ya Kiswahili au Kiingereza **tofauti na hapo maombi hayo hayatapokelewa.**
- Kichwa cha barua ya maombi kitaje nafasi ya kada unayoomba kwa ufasaha.
- Barua ya maombi isainiwe na mwombaji mwenyewe tofauti na hivyo maombi hayo **yatakataliwa**
- Uwasilishaji wa taarifa na sifa za kughushi wahusika watachukuliwa hatua za kisheria.
- Waombaji watakaokidhi sifa na vigezo watajulishwa tarehe ya usaili kupitia mbao za matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda, website ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda ambayo ni *www.bundadc.go.tz*, namba zao za simu na anuani walizotumia kwenye barua ya maombi ya kazi.
- **Barua zitumwe kwa njia ya Posta au ziwasilishwe kwa mkono masijala ya wazi ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda (Kata ya Kibara) kuanzia saa moja na nusu (1:30) asubuhi hadi saa tisa na nusu (09:30) alasiri.**



CamScanner

- Mwisho wa kutuma maombi ya kazi ni tarehe 14 Machi 2024.
- Maombi yote ya kazi yatumwe kwa anuani ifuatayo:-

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Bunda,
S.L.P 126,
**BUNDA - MARA**

Tangazo hili limetolewa na:-

........................

*Changwa M. Mkwazu*
Mkurugenzi Mtendaji (W)
BUNDA D.C

MKURUGENZI MTENDAJI (W)
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUNDA

Nakala:-

" Tovuti ya Halmashauri ya Wilaya ya Bunda www.bundadc.go.tz

" Mbao za Matangazo za Halmashauri ya Wilaya ya Bunda.



CamScanner